IBO IB DIPLOMA PROGRAMME
PROGRAMME DU DIPLÔME DU BI
PROGRAMA DEL DIPLOMA DEL BI



**SWAHILI B – HIGHER LEVEL – PAPER 1**
**SOUAHÉLI B – NIVEAU SUPÉRIEUR – ÉPREUVE 1**
**SWAHILI B – NIVEL SUPERIOR – PRUEBA 1**

Tuesday 2 November 2004 (morning)
Mardi 2 novembre 2004 (matin)
Martes 2 de noviembre de 2004 (mañana)

1 h 30 m

---

TEXT BOOKLET – INSTRUCTIONS TO CANDIDATES

- Do not open this booklet until instructed to do so.
- This booklet contains all of the texts required for Paper 1.
- Answer the questions in the Question and Answer Booklet provided.

LIVRET DE TEXTES – INSTRUCTIONS DESTINÉES AUX CANDIDATS

- N'ouvrez pas ce livret avant d'y être autorisé(e).
- Ce livret contient tous les textes nécessaires à l'épreuve 1.
- Répondez à toutes les questions dans le livret de questions et réponses fourni.

CUADERNO DE TEXTOS – INSTRUCCIONES PARA LOS ALUMNOS

- No abra este cuaderno hasta que se lo autoricen.
- Este cuaderno contiene todos los textos para la Prueba 1.
- Conteste todas las preguntas en el cuaderno de preguntas y respuestas.

**KIFUNGU A**

# REGINA MWANA WA ZANZIBAR WA EXTRA BONGO AWA GUMZO

Na Abdul Mitumba, Makumbusho

❶ KIBAO 'Regina Mwana wa Zanzibar', 'Jirani' na 'Walimwengu Remix' vya bendi mpya ya Extra Bongo, vimekuwa gumzo baada ya kutikisa ukumbi wa Makumbusho Village uliopo Kijitonyama.

❷ Extra Bongo ilifanya onyesho lake katika ukumbi huo siku ya jumamosi, ambapo pamoja na vibao hivyo, vibao vingine kama 'Extra Bongo 3×3' na 'Flora' pia vilifanikiwa <u>kuchengua mashabiki</u> waliofika kwa wingi ukumbini humo.

❸ Hilo lilikuwa onyesho lake la nne tangu ilipozinduliwa Desemba 26 katika ukumbi wa Diamond Jubilee, sambamba na utambulisho wa vibao vyake vinne vinavyounda albamu ya kwanza.

❹ Kumbi nyingine ambazo Extra Bongo imefanikiwa kutumbuiza ni TTC Chang'ombe, Friends Comer-Manzese na Mango Garden, Kinondoni.

❺ Akizungumza katika onyesho hilo, Mkurugenzi mtendaji wa bendi hiyo inayotumia mtindo wa kujinafasi, Ally Choky alisema lengo lao ni kuifanya bendi kuwa miongoni mwa <u>bendi zinazotamba</u> ndani na nje ya nchi.

❻ Alisema hatua yao ya kupiga karibu katika kila kumbi inalenga kujitangaza na baadaye ndipo itatangaza upi utakuwa ukumbi wake wa nyumbani.

❼ Katika hali iliyoonyesha kukubalika haraka kwa bendi hiyo, wapenzi walicheza karibu kila wimbo bila kujali wamewahi kuusikia au kuuona katika vituo vya televisheni.

**KIFUNGU B**

# AJIRA SIKU HIZI

❶ Naanza kwanza kutoa, ajira maana yake
Ndipo mbele kuendea, yaliyomo ndani yake
Ili kwa watoto pia, wasome ieleweke
Ajira hivi sasa, ni ngumu kupindukia.

❷ Kazi yoyote halali, ikupatiayo kipato
Yako si yako shughuli, ya kuomba au mwito
Ama ni ya Serikali, ilimradi kipato
Ajira kwa hivi sasa, ni ngumu kupindukia.

❸ Si kama ilivyokuwa, hapo zamani jamani
Wasomi walitanuwa, kubembelezwa kazini
Waso soma walipewa, kufanya serikalini
Ajira kwa hivi sasa, ni ngumu kupindukia.

❹ Mifano michache natoa, wale walimu wa Upe
Jeshi la kujitolea, mwishowe kazi wawape
Mashamba kuendelea, kwa weusi na weupe
Ajira kwa hivi sasa, ni ngumu kupindukia.

❺ Mtu katoka chuoni, uraiani kufika
Bure akaa nyumbani, pasipo kazi hakika
Wajaa serikalini, wafanyakazi hakika
Ajira kwa hivi sasa, ni ngumu kupindukia.

❻ Taarifa gazetini, mfanyakazi wataka
Yasema zingatieni, yafuatayo twataka
Ni elimu ya chuoni, uzoefu bila shaka
Ajira kwa hivi sasa, ni ngumu kupindukia.

❼ Kinachosemwa kwa sasa, ni sisi kujiajiri
Ni mitaji tumekosa, tunayo elimu nzuri
Zana twakosa kabisa, kwa vipi kujiajiri
Ajira kwa hivi sasa, ni ngumu kupindukia.

❽ Ni hapa napokoma, tujitahidi sana
Kujiajiri nasema, ukata kuepukana
Tatizo dunia nzima, Ulaya hadi Uchina
Ajira kwa hivi sasa, ni ngumu kupindukia.

**KIFUNGU C**

# TIBA MBADALA: KITUNGUU SAUMU HUTIBU MAGONJWA 40!

❶ Wiki hii katika safu hii, gazeti la Kiu lilitembelewa na daktari maarufu wa Tiba Mbadala jijini Dar, Dr Keffa ambaye pamoja na mambo mengi alielezea namna kitunguu saumu kinavyotibu maradhi mbalimbali.

❷ Dr Keffa ambaye anamiliki kliniki ya Tiba Mbadala iitwayo Upendo wa Mungu iliyopo Mwenge Mpakani jijini Dar, alisema vitunguu saumu vina vitamini C na madini mengi kama vile allesion, sulphur, phosphorous, ambayo hufanya kazi maalum ya kutuliza mfumo wa fahamu mwilini (nervous system). Alisema kuwa, vitunguu saumu hutibu zaidi ya maradhi 40 yamsumbuayo mwanadamu.

❸ "Baadhi ya maradhi yanayotibiwa na vitunguu saumu in kama vile uambukizo kwenye njia ya hewa (bronchitis), kuharisha, matatizo ya mishipa ya damu, minyoo tumboni na bawasiri (haemorrhoids)," alisema Dr Keffa ambaye pia hutibu ugumba, vidonda vya tumbo, kisukari, shinikizo la damu, pumu (asthma) na magonjwa mengine sugu kwa njia ya Tiba Mbadala.

❹ Aliyataja magonjwa mengine yanayotibiwa na kitunguu saumu kuwa ni mishipa ya damu ya vena kuota na kujikunja juu ya ngozi (varicose veins), maradhi ya figo, mawe kwenye mfuko wa nyongo (gall stones), kuumwa kichwa, kuondoa kitambi, chunusi, magonjwa ya ngozi, mnepo (hysteria), mfadhaiko wa akili, kukosa choo, homa ya matumbo (typhoid fever), magonjwa ya ini, wengu, matatizo ya kuona, kukosa hamu ya kula, kikohozi, sauti kukwaruza, uambukizo kwenye mapafu na jipu kwenye mapafu (pulmonary abscess), pumu (asthma) na mengineyo. Aidha alisema kuwajuisi ya kitunguu saumu huondoa aina zote za minyoo tumboni. Pia hutibu majipu, matatizo ya kukojoa, shinikizo la damu, kuhara damu, kipindupindu, tumbo kuuma na kunyonga pamoja na kuharisha.

❺ Pia aliongeza kuwa kula kitunguu saumu kikonyo kimoja kutwa mara tatu hutibu mafindofindo (tonsillitis), n.k.

❻ "Kitunguu saumu kina dawa ya kuua wadudu (antibiotic) inayoitwa illium ambayo ina uwezo wa kuua vijimelea vya magonjwa ambavyo husababisha ugonjwa wa ngozi, majipu, usaha na fangasi, mguuni," alisema. Kwa kutibu fangasi, alisema mgonjwa aponde kitunguu saumu apake kwenye unyayo na vidole vya miguu usiku anapokwenda kulala. Kwanza osha na uikaushe miguu.

## MATAYARISHO YAKE:

❼ Unaweza kukimenya kitunguu saumu na kukitafuna pamoja na chakula wakati wa kula. Chukua vibonge 10 hadi 20 vya kitunguu saumu, vimenye, kisha vipondeponde, kisha vichanganye na juisi ya malimao. Iache ikae hivyo usiku wote hadi asubuhi. Koroga vizuri ndipo uitumie. Tumia kikombe kidogo cha juisi hiyo asubuhi na jioni, usiache kijiko ulichokorogea katika juisi, kitafanya sumu. Ila ukitumia kijiko, kioshe. Njia nyingine ni kuchemsha mchanganyiko wa juisi ya malimao na kitunguu saumu na kutumia. Pia endelea kula saladi ya kitunguu saumu wakati wa chakula.

❽ "Kitunguu saumu kina harufu kali ambayo watu wengi hawaipendi, ili kuondoa hiyo harufu, kunywa pia maziwa," alifafanua Dr Keffa. Alisema Warumi wa zamani walitumia sana vitunguu saumu kwa sababu viliwapa kinga ya kutopata maradhi na kuwaongezea nguvu kwa maaskari. Alisema kila walipokuwa wakiondoka kwenda kwenye kazi ngumu au safari ndefu, walipewa juisi ya kitunguu saumu ili wahimili uchovu.

❾ "Ukiwa na ugonjwa wa ngozi, saga kitunguu na uweke katika eneo hilo. Funga na bandeji safi, acha kwa nusu saa kisha endelea kufanya hivyo kwa wiki mbili, utapona," alisema Dr Keffa.

❿ Ukiwa na vidonda alisema tiba yake ni kuponda kikonyo kimoja au viwili vya kitunguu saumu, kisha changanya na asali, matone kidogo, ongeza mafuta ya mawese, ponda jani la mti wa muarobaini, kamulia pale matone yake, changanya. Safisha vizuri kidonda, kwenye kidonda tia mchanganyiko huo, funga kwa bandeji safi. Safisha na kuweka tena mchanganyiko huo kila unapoona inafaa, hadi upone.

**KIFUNGU D**

# REVINA KUZINDUA 'NSENENE' DESEMBA 12




Mwanadada anayeibukia katika ngoma za asili, Revina Kasabila, anatarajia kuzindua albamu zake mbili, 'Nsenene' na 'Gulioni Katerero', Desemba 12, mwaka huu.

Uzinduzi wa albamu hizo, kila moja ikiwa na nyimbo sita, unatarajiwa kufanyika kwenye ukumbi wa vijana, Kinondoni, Dar es Salaam.

Akizungumza jana na waandishi wa habari kwenye Ukumbi wa Idara ya Habari (MAELEZO), Dar es Salaam, Revina alisema ya kuwa amekwisha anza maandalizi kwa ajili ya uzinduzi huo.

"Maandalizi yameanza, najua muda unatosha, hivyo bado ninaendelea na mazoezi kwa ajili ya uzinduzi," alisema.

Alizitaja nyimbo zilizo katika albamu ya 'Nsenene', zote zikiwa katika lugha ya Kihaya kuwa ni 'Nonyenda Iwe', 'Ahansi Ha', 'Nayorobana', 'Okutahulila Kwakwe', 'Omukama Rukamba.'

Kwa upande wa albamu ya 'Gulioni la Katerero' inayosifia gulio la Katerero lililopo Kagera vijijini, ina nyimbo za 'Omukaikulu ma Karungi', 'Mwanamke sura', 'Omwana Okwomomwesiga', 'Ensi Yawa', 'Nsenene Remix' na 'Gulioni Katerero' yenyewe.

Mwanadada huyo alisema kuwa baadhi ya nyimbo zitakuwa na maneno ya Kiswahili kwa lengo la kuifikishia jamii ujumbe.

Naye msimamizi wa uzinduzi huo, Juma Mbizo, alisema ya kuwa anatarajia kuwa uzinduzi huo utasindikizwa na wasanii wa miondoko ya Hip hop ambao watatangazwa hapo baadaye. Kwa mahojiano zaidi juu ya uzinduzi Juma aliwapatia waandishi wa habari anuani ya bendi na pia ya Idara ya Habari (MAELEZO) kama: Nsenene, S.L.P. 230, Dar es Salaam. Nambari ya simu: 03 911 614. Anuani ya ukumbi ilikuwa: Idara Habari (MAELEZO), S.L.P. 500, Dar es Salaam. Nambari ya simu: 03 892 771.